

# Zaidi ya mil. 300/- zatumika kununua boti za uvuvi

## Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imenunua boti 16 na injini 12 zenyet thamani ya Sh. milioni 395 zitakazotumiwa na maofisa uvuvi katika kudhibiti rasilimali za uvuvi nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema hayo jijini Mwanza alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi boti kwa maofisa wafawidhi wa uvuvi kwa Kanda za Ziwa Victoria, Tanganyika, Kanda ya Bahari ya Hindi, Kaskazini Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Waziri Ndaki alisema boti na injini hizo zimenunuliwa na serikali ili kuiwezesha wizara na watalaam wake kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia, kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini. Alizionba halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa hivyo ili kudhibiti rasilimali za uvuvi dhidi ya watu wanaojihusisha na uvuvi haramu.

"Halmashauri zetu zilizo kwenye mwambao wa bahari/ziwa na mito ziširikiane na wizara ili kwa pamoja tudhibiti uvuvi haramu amba bado ni changamoto kwa sasa," alisema.

Pia, alisema serikali itawashughulikia wavuvi haramu wote na kuwafikisha kwenye vyombo yya sheria.

Aliwataka wavuvi nchini kuhakikisha

kuwa wanalinda rasilimali za uvuvi ili zisiharibiwe na watu wanaojihusisha na shughuli za uvuvi haramu.

Aliwataka maofisa uvuvi waliokabidhiwa boti na injini hizo kuzilinda na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dk. Rashid Tamatamah, alisema shughuli za uvuvi nchini hufanyika katika maji baridi na bahari na kiasi kikubwa zikihuisha wuvuvi wadogo.

Alisema mwaka 2021 wavuvi wadogo 194,804 walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 57,991 na kuwezesha kuvuna tani 477,019 za samaki zenyet thamani ya Sh. trilioni 2.8 na tani 302,827.9 sawa na asilimia 63.0 zilitoka Ziwa Victoria.

Vilevile, uvuvi huo ulihusisha tani 42,302 na samaki hai wa mapambo 181,268 zenyet jumla ya thamani ya Sh. bilioni 414.23.

"Kati ya tani za samaki zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi, tani 36,657.46 sawa na asilimia 86.7 zilitoka Ziwa Victoria," alisema.

Dk. Tamatamah amefafanua kuwa ili uzalishaji wa samaki pamoja na mapato yake kwenye ziwa hili yaye endelevu, ajira zinazotokana na shughuli za uvuvi kwenye ziwa ziwe endelevu, miundombinu ya uvuvi iliyowekezwa na serikali

na watu binafsi iweze kufanya kazi kwa muda mrefu na manufaa yatokanayo na shughuli za uvuvi kwenye ustawi wa jamii yaye endelevu, wananchi hawana budi kulinda na kuzisimamia ipasavyo rasilimali za uvuvi pamoja na mazingira zinakofanyika shughuli za uvuvi.

Alisema katika juhudzi za wizara kusimamia rasilimali za uvuvi, iliunda kanda kuu nne za usimamizi wa rasilimali za uvuvi ambazo ni Kanda ya Ziwa Victoria, Kanda ya Ziwa Tanganyika, Kanda ya Bahari ya Hindi na Kaskazini Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zenyet jumla ya vituo 36 vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi.

Mkuu wa Mkoaa wa Mwanza, Robert Gabriel ameipongeza Wizara ya Mifugo na uvuvi kwa hatua hiyo ya kununua vifaa hivyo ambavyo vitasaidia katika kudhibiti na kupambana na wavuvi haramu mkoani Mwanza na nchini kwa ujumla.

Akitoa shukurani kwa niaba ya maofisa ufawidhi wa uvuvi walipokea vifaa hivyo, Ofisa Mfawidhi kutoka Kanda ya Bahari Hindi na Kaskazini Mashariki, Mathayo Werema, aliishukuru serikali kwa ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo watavitumia katika kudhibiti, kulinda rasilimali za uvuvi, pia kutoa elimu kwa jamii kuondokana na vitendo vya uvuvi haramu.